Hakuona Kitu Ila Majani

(Nothing But Leaves)

Na

Ellis P. Forsman

Hakuona Kitu Ila Majani

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 13, 2011

Hakuona Kitu Ila Majani

Marko 11:12-14

Marko 11:12-14, "*Hata asubuhi yake walipotoka Bethania aaliona njaa. Akaona kwa mbali mtini wenye majani, akaendaa ili labda aone kitu juu yake; na alipoufikilia hakuona kitu ila majani maana si wakati wa tini. Akajibu akauambia, taangu leo hata milele mtu assile matunda kwako. Wanafunzi wake wakasikia.*"

Marko hapa anaandika tabia za kibinadamu za Yesu – "*aliona njaa*" (ms.12).

Njaa ilikuwa ni sehemu ya dhihaka yake. Hata kama alikuwa Mkate wa Uzima, lakini bado aliona njaa; hata kama alikuwa maji ya uzima, lakini bado aliona kiu.

Mark 11:13, "*Akaaona kwa mbali mtini wenye majani akaenda ili labda aone kitu juu yake;…*"

Miti ya tini ilikuwa mingi huko Bethania.

"*Kuwa na majani*" juu yake ilikuwa ni ishara ya kuwa na matunda juu yake pia, kwa sababu matunda huonekana kabla ya majani.

Marko 11:13, "*...na alipoufikilia hakuona kitu ila majani…*"

Ingeweza kutarajiwa kwamba juu ya mti huu, na majani yake yalivyostawi kungeweza kupatikana matunda yaliyoiva. Hivyo Yesu, akaufikilia mtini kwa njaa yake, akitarajia kupata tunda. Lakini kwa mshangao wake mkuu "*hakuona kitu ila majani…*"

Yesu aliufikilia mti huu wa mzeituni ikiwa na majani mengi, lakini badalaa ya tunda, ilisimama mbele yake umbile la taifa la Kiyahudi, ikiwa na sura ya majani, lakini haizai matunda.

Marko 11:13, "*...maana si wakati wa tini.*"; "*Maana haikuwa wakati waa tini*" (Toleo lingine)

Hiyo ni, haikuwa wakati wa tini kuiva kikamilifu, sio wakati wa kuyavuna, sio wakati wa kawaida wa tini kuiva.

Matunda katika mti wa tini hujitengeneza kabla ya majani na inapaswa kujaa kabla ya majani hayajaonekana; hivyo mti huu kwa kujiandaa wenyewe kabla ya wakati wa tini, ilikuwa ni kujitangaza wenyewe kuwa ni mkuu kuliko miti mingine ya tini.

Hii iliifanya kuwa ishara ya kipigo kwa mnafiki, ambao hawaridhiki na muonekano wa kuwa wema kama watu wengine, mara nyingi huvaa muonekano wa kuwa bora.

Alafu, Yesu aliulaani mti huu wa tini. Marko 11:14, "*Akajibu akauambia tangu leo hata milele mtu asile matunda kwako. Wanafunzi wake wakasikia.*"

Kifungu chetu kinaleta mambo matatu:

- Alichokitafuta Yesu na kukipata.
- Alichokitafuta Yesu na kukipata.
- Alichokifanya Yesu na atafanya.

Alichokitafuta Yesu na kukipata

Matunda.

Ya mti wa tini – matunda.

Alikuwa na haki ya kuitarajia kwa sababu ilionyesha majani yake, ishara ya baadhi ya matunda.

Kwa taifa la Kiyahudi – matunda.

Alikuwa na haki ya kutarajia kwa saababu Mungu alifanya Israeli "*watu wake hasa.*"

Kumb. 7:6, "*Kwa maana wewe u taifa takatifu kwa BWANA, Mungu wako; BWANA Mungu wako amekuchagua kuwa watu wake hasa, zaidi ya mataifa yote walioko juu ya uso wa nchi.*"

Aliwajali na kuwalinda kwa uwezo wake. Kwa Wakristo leo – tunda.

Yohana 15:8, "*Hivyo hutukuzwa Baba yangu, vile mzaavyo sana nanyi mtakuwa wanafunzi wangu.*"

Leo, Bwana anapoliangalia kanisa chini kutoka mbinguni, alitaraajia matunda ya maisha ya wanafunzi wake, lakini wakati mwingine hapati "*kitu isipokuwa majani.*"

- Yohana 15:2, "*Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha ili lizidi kuzaa.*"
- Yohana 15:5, "*Mimi ni mzabibu ninyi ni matawi, akaaye ndaani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.*"

Hivyo basi, tunapomwona Mkristo leo tunatarajia kuona matunda ndani yake.

Tunatarajia kuona kiumbe kipya.

- 2 Kor. 5:17, "*Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.*"
- Efe. 4:22-24, "*Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; naa mfanywe wapya katika roho na nia zenu; mkavae utu mpya ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.*"

Tunatarajia kuona mfanano na sura ya Kristo.

- Fil. 2:5, "*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu;*"
- Rum. 8:9, "*Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.*"
- 1 Pet. 2:21, "*Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu akawaachia kielelezo mfuate nyayo zake.*"

Tunatarajia kuona tabia takatifu.

1 Pet. 1:15, "*Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote;*"

Takatifu – takaswa, safi, ametengwa na dhambi.

Tunatarajia kuona kujikana.

Luka 9:23, "*Akawaambia wote mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe ajitwike msalaba wake kila siku anifuate.*"

Bwana wetu ana njaa na matunda yaliomo ndani yetu; ana shauku ya kutuona tunafaa katika huduma yake.

Alichokitafuta Kristo na kukipata

Hakuna kitu isipokuwa majani.

Kwenye mti wa tini – "*hakuna kitu isipokuwa majani*."

Kwa taifa la Kiyahudi – "*hakuna kitu isipokuwa majani*." Mat. 23:25-28, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na chano, na ndani yake vimejaa unyang'anyi na kutokuwa na kiasi. Ewe Farisayo kipofu safisha kwanza ndani ya kikombe ili nje yake nayo ipate kuwa safi. Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu na uchafu wote. Vivyo hivyo ninyi nanyi kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenye haki, bali ndani mmejaa unafiki na maasi.*"

Kwa Wakristo leo – kwa baadhi bado hapati "chochote isipokuwa majani."

Tujichunguze wenyewe hapa:

Tunatabiri "kuihubiri Biblia". 1 Pet. 4:11, "*Mtu akisema na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu, ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu una yeye hata milele na milele. Amina.*"

Hii inahitaji kujifunza.

- 2 Tim. 2:15, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kaazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*"
- 1 Pet. 3:15, "*Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na hofu.*"

Lakini, je unafahamu inachofundisha Biblia?

Kama hujui, wewe "*hakuna kitu isipokuwa majani*".

Tunadai kushiriki meza ya Bwana kila siku ya Bwana.

Mdo. 20:7, "*Hata siku ya kwanza tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane.*"

Je unajaribu kuwafundisha wengine hili, alafu unaacha kuiweka katika utendaji? Katika siku ya Bwana, je unakaa nyumbani na kuwakaribisha wageni, au unajihusisha na mambo mengine? Kama ndivyo, basi wewe "si kitu isipokuwa majani".

Tunadai kumwabudu Mungu "katika roho na kweli".

Yohana 4:24, "*Mungu ni Roho nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*"

Wengine uenda ibadani, lakini hawaabudu. Wanadhani kwamba kwenda katika sehemu za ibada, na kukaa kwa muda mrefu, na kutoka nje tena ni ibada; alafu wanakosea mfumo wa ibada.

Wengine hawajali kushiriki meza ya Bwana; hawataki kuikosa; lakini pia hawashiriki ipasavyo. 1 Kor.11:27-29, "*Basi kila aulaye mkate huo au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mtu ajihoji mwenyewe na hivyo aule mkate na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake kwa kutokuupambanua ule mwili.*"

Wengine hupinga kwamba tunapaswa "*kila siku ya kwanza ya juma … aweke akiba,*" lakini hawatoi "*kama Mungu alivyowafanikisha*". 1 Kor. 16:2, "*Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake ili kwamba michaango isifanyike hapo nitakapokuja;*"

"*Kuweka akiba*" haimanishi "kuweka nyumbani", bali "kuweka kwenye hazina". Tafsiri ya NIV ilidhihakiwa kwa nguvu na wasomi wa Biblia kwa kuonyesha kwamba ilikuwa ni hakiba ya nyumbani.

"*Kila siku ya kwanza ya juma" kwa Kiyunani inamanisha,* "*Kila siku ya kwanza ya kila juma.*"

Au wanatoa kwa kukusudia. 2 Kor. 9:7, "*Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu.*"

Wengine wanawekaa msimamo kwamba tunapaswa kumsifu Mungu kwa nyimbo bila kuwa na matumizi ya vyombo vya muziki; wakati "*hawaimbi kwa roho na uelewa*". Efe. 5:19, "*Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu.*"

Wengine husifia mahubiri, lakini hawafaidi kwa kutoiweka katika vitendo.

Kwa yote haya "*si chochote isipokuwa majani*".

Wapo wale, walioko ndani na nje ya kanisa, ambao hujilaumu bila kuwa na toba.

Wengi huelewa mahubiri inayotafuta moyo, wanahuzunika kwa ajili ya dhambi, lakini bado hawajawa na nguvu ya hitaji ya kuziacha.

- Wanasema samahani, lakini bado wanaendelea na hali ya dhambi.
- Wanabadilika bila tendo.
- Wana matakwa, lakini mara nyingi ni kwa wakati ujao.

Wanaona sawa, lakini mara nyingi wanaruhusu uovu kuziongoza. Watu kama hao "*hawana kitu isipokuwa majani*."

Alichofanya Kristo na atakachofanya?

Kwa mti wa mzeituni – aliulaani na ukanyauka na haikuzaa matunda milele baada ya hapo.

Kwa taifa la Kiyahudi – walitupiliwa mbali. 1 Fal. 9:6-9, "*Bassi mkighairi mkaacha kunifuata ninyi na watoto wenu msizishike sheria zangu na amri zangu, nilizoziweka mbele yenu, tena mkienda na kuitumikia miungu mingine na kuiabudu, basi nitawakatilia Israeli mbali na nchi hii niliyowapa; na nyumba hii niliyoitakasa kwa jina langu nitaitupilia mbali na macho yangu, na Israeli watakuwa mithali na neno la tusi katika mataifa yote. Na ijapokuwa nyumba hii imetukuka namna hii, lakini kila apitaye atasituka na kuizomea; nao watasema kwa nini BWANA ameitenda nchi hii na nyumba hii mambo haya? Na watu watajibu kwa sababu wamemwacha BWANA Mungu wao, aliyewatoa baba zao katika nchi ya Misri, wakashikamana na miungu mingine na kuiabudu na kuitumikia, basi ndiyo sababu BWANA ameleta mabaya haya yote juu yao.*"

Hivyo, Israeli walitawanyika katika pande zote nne za dunia.

Kwa Wakristo wasio na faida – wamechomwa. Yohana 15:1-6, "*Mimi ndiye mzabibu wa kweli na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha ili lizidi kuzaa. Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia. Kaeni ndani yangu nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa pekeake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu ninyi ni matawi akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote. Mtu asipokuwa ndani yangu hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea.*"

Hapa tunajifunza hatima ya Mkristo mwaminifu na asiyemwaminifu.

Hitimisho

Vipi kuhusu maisha yako? Je yanazaa matunda, au ni tupu na tasa?

Kama Kristo angerudi leo na kutuangalia na kuona umahiri wetu, mtazamo mkuu wa majani, alafu hakuna matunda, matokeo yatakuwa ni nini?

Kama hilo ndio swala, hatasema kama ilivyoandikwa katika Mat. 25:23, "*Bwana wake akamwambia vema mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache nitakuweka juu ya mengi; ingia katika raha ya bwana wako.*"

Lakini angesema, kama ilivyoandikwa katika Mat. 25:41, "*Kisha atawaambia na wale walioko katika mkono wake wa kushoto, ondokeni kwangu mliolaaniwa mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari ibilisi na malaika zake.*"

Tunapaswa kutetemeka kabla moyo haujakutana na macho ya Mungu.

Tunapaswa kukumbuka kwamba kwa neema ya Mungu tunaweza kuwa waaminifu katika kumtumikia pia. 1 Kor. 15:10, "*Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo; na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nazidi sana kufanya kazi kupita wao wote; wala si mimi bali ni neema ya Mungu pamoja nami.*"